

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Barua pepe : press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

Paris
15 Mei, 2024

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amefanya uteuzi wa viongozi kama ifuatavyo:

- i) Amemteua Prof. Masoud Hadi Muruke kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu. Prof. Muruke anachukua nafasi ya Prof. Willy Lazaro Komba ambaye amemaliza muda wake.
- ii) Amemteua Bw. Ishmael Andulile Kasekwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB). Bw. Kasekwa ameteuliwa kwa kipindi cha pili.
- iii) Amemteua Balozi Maimuna Kibenga Tarishi kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela. Balozi Tarishi anachukua nafasi ya Prof. Joseph Rwegasira Buchweishaija ambaye amemaliza muda wake.
- iv) Amemteua Bw. Martin Emmanuel Kilimba kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya Biashara Tanzania (TCB). Bw. Kilimba anachukua nafasi ya Dkt. Edmund Bernard Mndolwa ambaye amemaliza muda wake.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Zuhura Yunus'.

Zuhura Yunus
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

